# KILIO CHANGU UKIKISIKIA

*F.A.Nyundo*







2.Ee Mungu wangu ndiwe kimbilio,
Ewe Bwana wangu ndiwe tegemeo,
Nikitaabika uje kwangu mbio,
Ewe ngome yangu njoo kwangu njoo.

3.Usinitupe wewe ndiwe kinga,
Mimi ni kondoo wewe wanichunga,
Adui zangu zidi kuwapinga,
Na giza likija nipatie mwanga.

4.Daima wewe ndiwe msaada,
Bwana usichoke zidi kunilinda,
Ukiwa nami sitapata shida,
Kwa uwezo wako mimi nitashinda.

5.Uniepushe na mwovu shetani,
Ili asinitie majaribuni,
Mimi mnyonge nakutumaini,
Wewe uwe nami nifike mbinguni.

6.Unitetee katika hukumu,
Unisaidie kwa mambo magumu,
Unisikie na unirehemu,
Unipe neema ziwe za kudumu.

..typed by Eleuter Massawe, March 2022, Nyamongo-Tarime, 0784462904.
Email: elepeter9@gmail.com